HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA | TOLEO NA: 001 | SEPTEMBA 2023

HALIUZWI

Jarida la

# FAHARI YA MKINGA

*Fahamu Zaidi*



## MHE.KINDAMBA AMESEMA SERIKALI YA MKOA ITAHAKIKISHA BEGA KWA BEGA HALMASHAURI YA (W) MKINGA INAKWENDA KUWA YAKUPIGIWA MFANO.

"Nyinyi mna mazingira rafiki ya kuifanya Mkinga kuwa kati ya halmashauri bora, mna ufukwe wa bahari, nimezungumza na ndugu yangu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Dkt. Hassan Abbas, amesema mkatenge maeneo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli za kitalii ambayo yatatuongezea mapato lakini pia yatatufanya mji wetu uchangamke zaidi".

Mhe. Waziri Kindamba

HABARI KAMILI UK.2



## "KASI NA UBORA WA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MIRADI UENDANE NA THAMANI YA FEDHA ZA MHE. RAIS SAMIA".

MKURUGENZI BI. ZAHARA MSANGI.

"Fedha hizi tulizoletewa ni nyingi sana, hivyo hatuna budi kutekeleza wajibu wetu ipasavyo ili kufikia matarajio ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufikisha maendeleo kwa Wananchi wote husuan wanaoishi vijijini, tukitekeleza miradi hii kwa wakati na ubora uliokusudiwa Watoto wetu watasoma vizuri, watafaulu na hatimaye tutaijenga Mkinga imara yenye maendeleo makubwa".

HABARI KAMILI UK.3



# MHE.KINDAMBA AMESEMA SERIKALI YA MKOA ITAHAKIKISHA BEGA KWA BEGA HALMASHAURI YA (W) MKINGA INAKWENDA KUWA YAKUPIGIWA MFANO.



**Na: Nassoro Rashid - MDC Habari**

Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Waziri Kindamba ameyasema hayo Juni 22, 2023 wakati akiongoza mkutano wa baraza maalum la hoja za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 uliofanyika katika ukumbi uliopo ndani ya jengo la Halmashauri ya (W) Mkinga.

Kupitia mkutano huo Mhe. Kindamba amesema wana kazi kubwa ya kubadili hali za kiuchumi za halmashauri na watu wake huku akisisitiza kuwa ajenda ya kuwawezesha kiuchumi ni ajenda namba moja ili baadae watathmini halmashauri zimeongeza kipato gani lakini na watu wake wameweza kuongeza kipato chao kwa namna gani.

"Nyinyi mna mazingira rafiki kabisa ya kuifanya halmashauri ya Mkinga kuwa kati ya halmashauri bora kabisa, mna ufukwe wa bahari, nimezungumza na ndugu yangu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Dkt. Hassan Abbas, amesema mkatenge maeneo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji wa mahoteli ya kitalii ambayo yatatuongezea mapato lakini pia yatatufanya mji wetu uchangamke zaidi". Alisema Mkuu wa Mkoa Mhe.Kindamba.

Sambamba na hilo Mkuu wa Mkoa ametumia baraza hilo kuzishukuru wilaya zote za Mkoa wa Tanga kwa kufuata maelekezo yake katika zoezi zima la mbio za mwenge wa uhuru 2023 kwa kufanikiwa kuzindua miradi yote ya maendeleo mkoani humo pamoja na kuwepo kwa mikesha ya aina yake.

# "KASI NA UBORA WA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MIRADI UENDANE NA THAMANI YA FEDHA ZA MHE. RAIS SAMIA". -MKURUGENZI BI. ZAHARA MSANGI.



**Na: Nassoro Rashid - MDC Habari**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga Bi. Zahara Abdul Msangi ameendelea kusisitiza Kasi na Ubora katika utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu ya Shule za Msingi inayotekelezwa katika vijiji mbalimbali kwenye Halmashauri kupitia fedha za Ruzuku toka serikali kuu.

Ameyazungumza hayo siku ya Jumamosi Agosti 12, 2023 wakati akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo ambapo alitembelea kwenye vijiji na kata mbalimbali za wilaya ya Mkinga kukagua maendeleo na kasi ya ujenzi kwa kuongozana na Afisa Elimu Msingi pamoja na Mhandisi wa Wilaya.

Aidha katika ukaguzi huo Bi. Zahara amesisitiza kuwa miradi ikamilike kwa wakati huku akisema ubora wa miradi hiyo iendane na thamani ya fedha zinazotumika.

Mkurugenzi huyo amesema Halmashauri ilipokea fedha jumla ya shilingi Bilioni 1.35 katika mwaka wa fedha 2022-2023 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu msingi lengo ikiwa ni kuimarisha na kuendeleza kasi ya maendeleo ya sekta ya elimu wilayani Mkinga.

"Fedha hizi tulizoletewa ni nyingi sana, hivyo hatuna budi kutekeleza wajibu wetu ipasavyo ili kufikia matarajio ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufikisha maendeleo kwa Wananchi wote hususan wanaoishi vijijini, tukitekeleza miradi hii kwa wakati na ubora uliokusudiwa Watoto wetu watasoma vizuri, watafaulu na hatimaye tutaijenga Mkinga imara yenye maendeleo makubwa". Alisema Bi. Zahara

Wakati huohuo Mkurugenzi Bi. Zahara amewataka Wananchi kushirikiana na viongozi kuanzia ngazi ya vijiji, Kata pamoja na Wilaya katika kutunza miradi yote ya maendeleo iliyopo na inayoendelea kujengwa katika maeneo yao ili iendelee kuwanufaisha kwa miaka mingi kama inavyokusudiwa.

....Inaendelea UK.4

......Inatoka UK.3



“Miradi yote hii kuanzia madarasa ya shule za msingi, sekondari, maji, afya, umeme pamoja na barabara inatumia fedha nyingi sana ambazo Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akituletea, hivyo napenda kutoa wito kwa Wananchi wote kuanzia ngazi ya vijiji, Kata na Wilaya tushirikiane kuitunza miradi hii ili iendelee kutunufaisha kwa miaka mingi, kwani uwepo wa miradi hii ni ufunguo wa kuleta maendeleo”. Aliongezea Bi. Zahara.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi amesema wataendelea kuhakikisha wanafungua milango ya wilaya kwa kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukuza ustawi wa utoaji wa huduma bora kwa Wananchi ambayo ni chachu ya maendeleo ya Mkinga.

# MKUU WA WILAYA YA MKINGA AWATAKA WAZAZI NA WALEZI KUTIMIZA JUKUMU LA ULINZI NA USALAMA KWA WATOTO.






Na: Nassoro Rashid
MDC Habari

Wito huo umetolewa kwa wazazi, walezi pamoja na vyombo vya usalama kuhakikisha jukumu la ulinzi na usalama kwa watoto linapewa kipaumbele kikubwa ili kuondokana na tabia zisizofaa zinazoweza kuchangia watoto kupata madhara.

Hayo yametanabaishwa Juni 16, 2023 na Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Mhe. Kanali Maulid Hassan Surumbu wakati wa kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika kiwilaya iliyofanyika katika ukumbi wa Halmshauri hiyo na kuhudhuriwa na watumishi, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, wazazi, pamoja na walimu.

Aidha katika hafla hiyo Mhe. Kanali Surumbu amesema maadhimisho hayo ni muhimu kwa kuweka alama ya ukombozi kwa mtoto wa kiafrika kutokana na kumbukizi ya maanda mano ya Soweto yaliyokuwa na lengo la kupinga unyanyasaji na unyimwaji haki kwa Watoto nchini South Afrika **Juni 16, 1976**.

> *"Nchi yetu leo hii inaungana na mataifa yote ya bara la Afrika kuadhimisha siku hii muhimu ikitilia mkazo kauli mbiu ya mwaka huu inayosema **'Zingatia Usalama wa Mtoto katika Ulimwengu wa Kidigitali'**".*
> *Alisema Mhe. Surumbu*

Sambamba na hayo Mhe. Kanali Surumbu ameagiza vyombo vya usalama kwa kushirikiana na jamii kuhakikisha wanaungana kwa pamoja kutokomeza unyanyasaji kwa watoto na kuchukua hatua stahiki za kisheria pale wanapobaini tatizo lolote lenye viashiria vya unyanyasaji na ukandamizaji wa haki kwa mtoto.

Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yamekuwa na mchango mkubwa kwa jamii katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa mtoto unachungwa hususani katika ulimwengu wa sasa ambapo sayansi na teknolojia imekuwa sehemu kubwa ya maisha hivyo jamii inapaswa kuhimizwa umuhimu wao ili kuzuia madhara yanayoweza kusababishwa na uwepo wa mfumo wa digitali.

# "UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI IENDANE NA USAMBAZAJI KWA WANANCHI".- MHE. KANALI SURUMBU





Na: Nassoro Rashid
MDC Habari

Kauli hiyo imesemwa Juni 21, 2023 na mkuu wa wilaya ya Mkinga Mhe. Kanali Maulid Hassan Surumbu wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa mradi wa usambazaji maji kutoka Mkinga - Horohoro wenye thamani ya **Billioni 35.4** unaojengwa na kampuni ya STC Ltd ulioanza Disemba 2022 na kutarajiwa kukamilika Novemba 2023.

Katika ziara hiyo Mhe. Surumbu alifanikiwa kutembelea ujenzi wa matanki 5 ya maji katika maeneo tofauti ili kuona maendeleo yake ambapo moja lipo katika kijiji Cha Mtimbwani lenye ujazo wa Lita 250000, Horohoro Lita 200000, Kilulu Duga, Manza pamoja na Kasera yote yakiwa na ujazo wa Lita 500000 kila moja.

Aidha Mhe. Surumbu amesema utekelezaji wa mradi huo uendane sambamba na usambazaji wa maji kwa Wananchi ili kurahisisha upatikanaji wake katika maeneo mengi na kuwanufaisha katika shughuli zao za kila siku baada ya kukamilika.

*"Tuhakikishe utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu unaenda sambamba na usambazaji wa maji kwa Wananchi ili uwafikie na kuwanufaisha pindi utakapokamilika". Alisema Mhe. Surumbu*

Hatua hii ya ujenzi wa miundombinu ya usambazi wa miradi ya maji yenye chanzo chake kutoka Mabayani Jijini Tanga kuja Mkinga - Horohoro ni muendelezo wa juhudi mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Wizara ya Maji kuhakikisha huduma hiyo inawafikia Wananchi wengi na kuwanufaisha katika shughuli zao za kila siku.



# "TUTAHAKIKISHA TUNAENDELEA KUSHIRIKIANA KUILETEA MAENDELEO MAKUBWA HALMASHAURI YA (W) MKINGA" -

Mhe. Amani J. Kasinya





**Na: Nassoro Rashid**
**MDC Habari**

Kauli hiyo imetolewa Agosti 17, 2023 na Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Mkinga Mhe. Amani Kasinya wakati akiongoza Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika katika ukumbi uliopo ndani ya jengo la ofisi za Halmashauri ikiwa ni mkutano wa kukamilisha mwaka wa fedha 2022 - 2023.

Mara baada ya kuhitimisha mkutano huo Mhe. Kasinya amesema kwa ujumla walilenga kujadili kwa namna gani wataendelea kuwa sehemu ya chachu ya maendeleo ya Wilaya ya Mkinga.

Inaendelea UK.8

....Inatoka UK.7

Aidha Mwenyekiti huyo amesema wao kama viongozi wana kila sababu ya kushirikiana kuimarisha uchumi wa Halmashauri kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato kwenye kata zao lakini pia kuelekeza nguvu katika kuinua kipato cha kila mwananchi kupitia fursa za kimaendeleo zilizopo ndani ya Halmashauri.

*“Tutahakikisha tunaendelea kushirikiana kuiletea maendeleo makubwa Halmashauri ya Mkinga, kwani uwepo wetu Madiwani, ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi na Timu yake ya Wataalamu ni hazina kubwa ya kusimika maono ya Mhe. Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa Wananchi wetu, na haya yatawezekana kwa kuendelea kuwaletea Maendeleo bora kuanzia ngazi ya vijiji hadi Wilaya”. **alisema Mhe. Amani Kasinya***

## MH.KADIRI FULIZA AMEENDELEA TENA KUAMINIWA KUWA MAKAMU MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA (W) YA MKINGA





Katika hatua nyingine Waheshimiwa Madiwani walifanya zoezi la uchaguzi wa kumchagua Makamu Mwenyekiti ambapo jumla ya waliojiandikisha kupiga kura walikuwa Madiwani 28 huku kura za ndio zikiwa 23 kura za hapana 2 na kura zilizoharibika 3.



Aidha mara baada ya kutanganzwa kuendelea na nafasi hiyo Mhe. Kadiri Fuliza ambaye pia ni diwani wa kata ya Manza amesema ataendelea kushirikiana nao pamoja kusimamia sheria, kanuni na misingi ya uongozi ili kuyafikia maendeleo yanayokusudiwa.

*“Niwashukuru sana kwa kuendelea kuniamini tena, umoja na mshikamano tulionao ni chachu ya kuendelea kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa vitendo, ni imani yangu kwamba tutaendelea kushirikiana kwa dhati kama awali kuhakikisha Halmashauri hii inapata Maendeleo makubwa tunayoyakusudia”. **- Alisema Mhe. Kadiri.***

Mikutano hii ya Baraza la Madiwani imekuwa ni sehemu muhimu ya kuibua, kuchagiza, kuimarisha pamoja na kuendeleza maono yenye tija kwa Halmashauri ya Mkinga ambayo inakua kwa kasi siku hadi siku kulingana na uwepo wa ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

# WITO WATOLEWA KWA WANAUME KUWAPA MUDA MZURI NA MAZINGIRA RAFIKI KWA WANAWAKE KUNYONYESHA WATOTO.





Na: Nassoro Rashid
MDC Habari

Halmashauri ya wilaya ya Mkinga kupitia Ofisi ya Mganga Mkuu kwa kushirikiana na wadau wa shirika la World Vision wametoa semina kwa wanaume kuhusu ushiriki wao katika unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa mtoto.

Semina hiyo imetolewa Agosti 07, 2023 katika ukumbi mdogo wa Shirika la World Vision uliopo wilayani humo ikiwa ni katika kuadhimisha kilele cha maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji kwa wanaume wenye watoto walio katika umri wa kunyonya ambao ni chini ya miaka miwili (2).

Awali akifungua semina hiyo Mganga Mkuu wa wilaya Dkt. Joseph Ligoha ameeleza kwa upana faida za unyonyeshaji kwa mama na mtoto zikiwemo kumuepusha mama na hatari ya kupata saratani pamoja na kumsaidia mtoto kukua vizuri kiafya na kiakili.

*"Semina hii imelenga kuwafundisha wanaume namna ya kuwajibika katika kusaidia wanawake wanaonyonyesha waweze kupata muda mzuri na mazingira rafiki ya kunyonyesha watoto ili waweze kukua vizuri kiafya".* Alisema Dkt. Ligoha

Ifahamike kuwa maadhimisho ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa mtoto Duniani yalianza tangu Agosti 01, 2023 na kuhitimishwa tarehe 07.08.2023 ikiwa na kauli mbiu ya "Saidia Unyonyeshaji, Wezesha Wazazi kulea Watoto na Kufanya kazi zao kila Siku".

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA

Septemba 25, 2023

## TAARIFA KWA UMMA

### MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI 1,354,050,000.00 KWA AJILI YA UJENZI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/ 2023.

Halmashauri ya wilaya ya Mkinga imepokea jumla ya fedha kiasi cha shilingi za Kitanzania Bilioni Moja Milioni Miatatu Hamsini na Nne na Elfu Hamsini (1,354,050,000.00) kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za Msingi kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| A: FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU | 639,250,000.00 |
| B: FEDHA ZA MRADI WA BOOST | 692,800,000.00 |
| C: FEDHA ZA MRADI WA LANES | 22,000,000.00 |
| **JUMLA YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ZILIZOPOKELEWA** | **1,354,050,000.00** |

**A:** Mchanganuo wa Mapokezi ya Fedha za miradi ya maendeleo **Ruzuku kutoka Serikali Kuu** ni kama ufuatao:-

Mapokezi ya shilingi Milioni Kumi na Moja (11,000,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika shule ya msingi Boma Subutuni iliyopo kijiji cha Boma Subutuni kata ya Boma, kadhalika mapokezi ya shilingi Milioni Kumi na Moja (11,000,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa matundu 10 shule ya msingi Kibiboni iliyopo kijiji cha Kibiboni kata ya Mtimbwani pamoja na shilingi Milioni Kumi na Moja (11,000,000.00) ujenzi wa matundu 10 ya vyoo shule msingi Kibago iliyopo kijiji cha Kuze Kibago kata ya Bosha.

Kadhalika mapokezi ya jumla ya shilingi Milioni Mia Moja (100,000,000.00) kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya Madarasa Matano (5) katika shule ya msingi Duga iliyopo kijiji cha Sigaya kata ya Sigaya pamoja na shilingi Milioni Mia Moja (100,000,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matano (5) shule ya msingi Maramba 'B' iliyopo kijiji cha Maramba 'A' kata ya Maramba.

Sambamba na mapokezi ya shilingi Milioni Ishirini na Tano (25,000,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 katika shule ya msingi Cheto iliyopo kijiji cha Gombero kata ya Gombero, pia shilingi Milioni Ishirini na Tano (25,000,000.00) ya ujenzi wa Madarasa 2 shule ya msingi Mkambani iliyopo kijiji cha Boma kata ya Boma, Milioni Ishirini na Tano (25,000,000.00) Madarasa 2 shule ya msingi Kilulu Duga iliyopo kijiji cha Kilulu Duga kata ya Sigaya, Milioni Kumi na Mbili na Laki Tano (12,500,000.00) ujenzi wa Darasa Moja (1) shule ya msingi Mavovo iliyopo kijiji cha Mavovo kata ya Bwiti, Darasa Moja (1) shule ya msingi Kigongoi iliyopo kijiji cha Vuga kata ya Kigongoi, Milioni Kumi na Mbili na Laki Tano (12,500,000.00) ya Darasa Moja (1)

Inaendelea UK.11


Simu: Na. 027-2660501
Fax: Na. 027-2660500
Barua pepe: Info@mkingadc.go.tz
Tovuti: www.mkingadc.go.tz

.....Inatoka UK.10

shule ya msingi Mbuta iliyopo kijiji cha Mbuta kata ya Mwakijembe, Milioni Ishirini na Tano (25,000,000.00) Madarasa Mawili (2) shule ya msingi Mtundani iliyopo kijiji cha Mtundani kata ya Manza pamoja na Milioni Kumi na Mbili na Laki Tano (12,500,000.00) ya Darasa Moja (1) shule ya msingi Horohoro Border iliyopo kijiji cha Horohoro Border kata ya Duga.

Pia mapokezi ya shilingi Milioni Ishirini (20,000,000.00) kwa ajili ya Ukamilishaji wa Bweni moja (1) la Watoto wenye mahitaji maalum pamoja na ujenzi wa uzio wa Bweni la Watoto wenye mahitaji maalum wenye thamani ya shilingi Milioni Thelathini (30,000,000.00) vyote katika shule ya msingi Maramba JKT iliyopo kijiji cha Maramba 'A' kata ya Maramba.

Ujenzi wa Nyumba Tatu (3) za Walimu aina ya (mbili kwa moja) maeneo tofauti ambapo shilingi Milioni Sitini na Tano (65,000,000.00) imepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba moja (1) katika shule ya msingi Bamba Estate iliyopo kijiji cha Kwangena kata ya Mnyenzani, shilingi Milioni Sitini na Tano (65,000,000.00)Nyumba moja (1) katika shule ya msingi Mkambani iliyopo kijiji cha Boma Subutuni kata ya Boma pamoja na shilingi Milioni Sitini na Tano (65,000,000.00) ya Nyumba 1 katika shule ya msingi Jasini iliyopo kijiji cha Mahandakini kata ya Mayomboni.

Jumla ya Fedha zilizotumika kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa wa miundombinu hii ni shilingi Milioni Kumi na Moja Laki mbili na elfu Hamsini tu (11,250,000.00).

Hivyo jumla ya Fedha zilizopokelewa Ruzuku toka Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ni shilingi **Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa Laki Mbili na Elfu Hamsini tu (639,250,000.00).**

**B:** Mchanganuo wa Jumla ya Mapokezi ya fedha za utekelezaji wa mradi wa BOOST ni kama ufuatao:-

Jumla ya kiasi cha shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini na Nane na Laki Tano (348,500,000.00) kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa shule mpya moja yenye mkondo mmoja (1) shule ya msingi Maramba JKT iliyopo kijiji cha Maramba 'A' kata ya Maramba.

Kadhalika jumla ya kiasi cha shilingi Milioni Mia moja Ishirini na Tano (125,000,000.00) kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa madarasa matano (5) katika shule ya msingi Mjesani iliyopo kijiji cha Mnyenzani kata ya Mnyenzani, Milioni Sabini na Tano (75,000,000.00) Madarasa 3 shule ya msingi Perani iliyopo kijiji cha Perani kata ya Mwakijembe pamoja na Milioni Hamsini (50,000,000.00) ya Madarasa 2 shule ya msingi Mtimbwani iliyopo kijiji cha Mtimbwani kata ya Mtimbwani.

Pamoja na jumla ya fedha kiasi cha shilingi Milioni Sitini na Tisa na Laki Moja (69,100,000.00) kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa madarasa mawili ya mfano ya Elimu ya Awali katika shule ya Mkungumize iliyopo kijiji cha Kisiwani 'A' kata ya Daluni.

Sambamba na hayo mapokezi ya fedha kiasi cha shilingi Milioni Kumi na Mbili na Laki sita (12,600,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo sita (6) katika shule ya msingi Mjesani

Inaendelea UK.12


Simu: Na. 027-2660501
Fax: Na. 027-2660500
Barua pepe: Info@mkingadc.go.tz
Tovuti: www.mkingadc.go.tz

.....Inatoka UK.11

iliyopo Kijiji cha Mnyenzani kata ya Mnyenzani, Matundu Matatu (3) ya vyoo yenye thamani ya shilingi Milioni Sita na Laki Tatu (6,300,000.00) katika shule ya msingi Mtimbwani iliyopo kata ya Mtimbwani pamoja na Matundu Matatu (3) ya vyoo katika shule ya msingi Perani iliyopo kijiji cha Perani kata ya Mwakijembe.

Hivyo jumla ya Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST ni shilingi Milioni Mia Sita Tisini na Mbili na Laki nane tu (692,800,000.00).

C: Mchanganuo wa jumla ya Fedha za mradi wa LANES ni kama ufuatao:-

Jumla ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya ukarabati/ Ujenzi wa Kituo kimoja (1) cha Walimu katika shule ya Msingi Uhuru iliyopo kijiji cha Maramba 'A' kata ya Maramba ni shilingi Milioni Ishirini (20,000,000.00) pamoja na fedha za ufuatiliaji ni shilingi Milioni Mbili (2,000,000.00) hivyo kupelekea jumla ya shilingi Milioni Ishirini na Mbili (22,000,000.00) kupokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa LANES kwenye kata hiyo.

Hivyo Uongozi wa Halmashauri ya Wiaya ya Mkinga unapenda kuufahamisha umma kuwa miradi yote iliyoainishwa tayari imefikia 97% ya ujenzi wake ambapo mengine imeshakamilika na baadhi ipo katika hatua za umaliziaji ili dhana ya kuimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma bora kwa Jamii uendelee,lengo kuifikia dhamira na makusudio mapana ya Serikali ya awamu ya sita (6) inayoongozwa na Mhe. Rais DKT. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mstari wa mbele kutuletea maendeleo bora kupitia ujenzi wa miundombinu ya sekta ya Elimu, Afya, Uchumi, Utalii, Barabara, Masoko, Kilimo na Ufugaji pamoja na mengine mengi yanayotekelezwa na Serikali ili kuwafikia Wananchi wake kwa uweledi uliotukuka.

Imetolewa na;

**NASSORO RASHID ISSA**
**KAIMU MKUU KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA (W) MKINGA**


Simu: Na. 027-2660501
Fax: Na. 027-2660500
Barua pepe: Info@mkingadc.go.tz
Tovuti: www.mkingadc.go.tz

## HABARI PICHA: MIRADI YA RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU



Nyumba ya Walimu aina ya mbili kwa moja (2x1) Shule ya Msingi Mkambani imejengwa kupitia Ruzuku toka Serikali Kuu ipo Kijiji cha Kichakamiba Kata ya Boma



Nyumba ya Walimu aina ya mbili kwa moja (2x1) Shule ya Msingi Jasini imejengwa kupitia Ruzuku toka Serikali Kuu ipo Kijiji cha Mahandakini Kata ya Mayomboni

## HABARI PICHA: MIRADI YA RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU



Vyumba vya Madarasa Matano (5) Shule ya Msingi Duga imejengwa kupitia Ruzuku toka Serikali Kuu ipo Kata ya Sigaya Wilaya ya Mkinga.



Vyumba vya Madarasa Mawili (2) na Chumba Kimoja cha Ofisi ya Walimu Kituo Shikizi Shule ya Msingi Cheto imejengwa kupitia Ruzuku toka Serikali Kuu ipo Kijiji cha Gombero Kitongoji cha Mwamkongo Pangarawe Kata ya Gombero.

## HABARI PICHA : MIRADI YA BOOST






Mradi wa Madarasa Matano (5) Shule ya Msingi Mjesani iliyopo Kata ya Mnyenzani Wilaya ya Mkinga



Mradi wa Madarasa Matatu (3) Shule ya Msingi Perani iliyopo Kata ya Mwakijembe Wilaya ya Mkinga

## HABARI PICHA : MIRADI YA BOOST





Mradi wa Shule ya Msingi Maramba JKT wenye Vyumba vya Madarasa 9 ikiwemo na Madarasa Mawili ya Awali, Ofisi za Walimu 2 pamoja na Jengo la Utawala




Mradi wa Vyumba Viwili vya Madarasa na Ofisi ya Walimu Shule ya Msingi Mtimbwani

## HABARI PICHA: MRADI WA LANES









Mradi wa ukarabati na ujenzi wa Kituo cha Walimu kilichopo Kijiji cha Maramba 'A' kata ya Maramba kimegharimu jumla ya shilingi Milioni Ishirini na Mbili (22,000,000) kupitia Mradi wa Lanes.

# KAMATI YA SIASA WILAYA YA MKINGA YARIDHISHWA NA UJENZI WA MIRADI YA BOOST





**Na: Nassoro Rashid**
**MDC Habari**

18/8/2023

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Mkinga Mhe. Abdallah S. Singano Agosti 18/8/2023 ameongoza Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya BOOST yenye thamani ya jumla ya shilingi Milioni 692,800,000 inayotekelezwa wilayani humo.

Katika ziara hiyo Kamati ilifanikiwa kufanya ukaguzi katika kata ya Mtimbwani, Mwakijembe, Daluni, Maramba, na Mnyenzani ikiwemo miradi mitano (5) ya ujenzi wa vyumba 19 vya madarasa, matundu 16 ya vyoo, ofisi za walimu pamoja na madarasa 2 ya mfano ya Elimu ya Awali.

Aidha akizungumza wakati wa majumuishio ya ziara hiyo Mhe. Singano amesema wameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa miradi hiyo yote na wanaamini itakuwa na manufaa makubwa kwa Wananchi pamoja na Wanafunzi.

> *"Tumeikagua miradi yote kwa umakini ambapo kwa sasa ipo katika hatua za ukamilishwaji wake, kiukweli Kamati hii imeridhishwa na ujenzi huu na tunampongeza sana Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea fedha hizi ndani ya Wilaya yetu, hakika Watoto wetu watanufaika kwa kupata elimu katika mazingira bora na salama yatakayoimarisha ufaulu wao."*
> *Alisema Mhe. Singano.*



Madarasa (2) na Ofisi-Shule ya Msingi Mtimbwani

Sambamba na hayo Kamati imewapongeza Viongozi wote wa Chama na Serikali kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata, Wilaya pamoja na Wataalamu wa Halmashauri kwa kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inaendelea kujengwa kwa kuzingatia thamani ya fedha na ubora ambapo itasaidia kuongeza ufanisi wa ukuaji wa maendeleo ya uchumi, elimu pamoja na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Katika hatua nyingine Mwenyekiti ameendelea kutoa wito kwa Wananchi kushiriki katika shughuli za ujenzi wa miradi ya maendeleo pale wanapohitajika lakini pia amezitaka Kamati za ujenzi kuhakikisha Miradi hiyo inakamilika haraka ili iweze kutumika kwa maslahi mapana ya Wilaya ya Mkinga.




# MATUKIO MBALIMBALI KWENYE MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU JUNI 12, 2023

**"TUNZA MAZINGIRA, OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"**






# MATUKIO MBALIMBALI KWENYE MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU JUNI 12, 2023

**"TUNZA MAZINGIRA, OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"**

















# "YOYOTE YULE ATAKAYEENDA KINYUME NA MAFUNZO MLIYOPEWA ATAWAJIBISHWA" - BI. ZAHARA MSANGI



Nassoro Rashid
MDC Habari

Msimamizi wa uchaguzi Jimbo la Mkinga Bi. Zahara Msangi amewataka Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura kutokwenda kinyume na mafunzo pamoja na maelekezo waliyoyapata.

Ametoa wito huo Julai 10, 2023 wakati akifungua mafunzo ya wasimamizi wa vituo kwa ajili ya zoezi la uchaguzi mdogo wa nafasi ya udiwani kata ya Bosha uliofanyika rasmi Julai 13 mwaka huu.

Bi. Zahara amesema msimamizi wa uchaguzi kazi yake kubwa ni kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za uchaguzi.

*"Haitakiwi kwenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi, hivyo yoyote yule ambaye atakayeenda kinyume na mafunzo mliyopewa atawajibishwa".*
*Alisisitiza Bi. Zahara*

Aidha ameongeza kuwa msimamizi wa uchaguzi anapaswa kufahamu vyema majukumu yake ili kuepusha muingiliano wa majukumu na Karani Muongozaji au Mlinzi hivyo amewataka kuwa watulivu katika mafunzo hayo na kuyapa umuhimu kwa kuzingatia maelekezo wanayopewa na Wawezeshaji.

Kadhalika Bi. Zahara amesema Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanya maandalizi yote muhimu kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Mkinga juu ya uchaguzi huo hivyo anaamini Wasimamizi hao watayatumia mafunzo hayo kufanikisha zoezi hilo kwa uweledi mkubwa.

Mafunzo ya Wasimamizi wa Vituo vya kupigia kura yameanza mara baada ya kukamilika kwa mafunzo ya Makarani Waongozaji ambayo yalifanyika kwa muda wa siku mbili.





# MSIMAMIZI WA UCHAGUZI AMEWATAKA WASIMAMIZI WA VITUO KUWA WATULIVU, KUJIAMINI NA KUSHIRIKIANA



Na:Nassoro Rashid
MDC Habari

Wito huo umetolewa na Msimamizi wa Uchaguzi jimbo la Mkinga Bi. Zahara Abdul Msangi wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya wasimamizi wa vituo vya uchaguzi yaliyokuwa yakifanyika katika ukumbi uliopo kwenye ofisi za Halmashauri ya wilaya ya Mkinga tangu Julai 10, 2023.

Akizungumza mara baada ya mafunzo hayo Bi. Zahara amewashukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa namna ambavyo wamekuwa wakijituma kuhakikisha mafunzo hayo yanafanyika na washiriki wanaelewa ipasavyo.

Aidha Msimamizi huyo amesema ameridhishwa na utolewaji wa mafunzo hayo kwa nadharia na vitendo ambapo imepelekea ufanisi

.....INAENDELEA UK. 23

.....INATOKA UK. 22

mkubwa wa uelewa kwa wasimamizi hao wa vituo.

*"Ni imani yangu kwamba kwa mafunzo haya kazi itakuwa nzuri na ya kupigiwa mfano, hivyo kila mtu akatumie uweledi wake,uwezo wake, kipaji chake kuhakikisha kwamba anafanya vizuri". Alisema Bi Zahara.*

Pia ametoa wito pamoja na kuwasisitiza Wasimamizi hao mambo matatu yakiwemo kujiamini kutokana na mafunzo waliyopewa, kufanya kazi kwa ushirikiano pamoja na kuwa watulivu ili kuhakikisha kazi watakayokwenda kuifanya inakuwa bora na yenye manufaa mema kwa Taifa.





*"Niwasisitize mkawe watulivu katika kazi mnayoenda kuifanya, kwani utulivu utakufanya uwe na uwezo mkubwa wa kutafakari lakini kutoa maamuzi sahihi, muwe makini na muwe tayari kushauriana ili kazi hii iwe na ufanisi". Alisisitiza Bi.Zahara.*

Sambamba na hayo amewataka kufika mapema kwenye vituo vyao vya kazi siku ya uchaguzi ili kuvikagua vifaa vyao pamoja na kuhakikisha kila kitu kinakaa sawa kabla ya zoezi la uchaguzi kuanza.



## HABARI PICHA: MATUKIO MBALIMBALI MAONESHO YA NANENANE MOROGORO





Mkurugenzi Mtendaji (W) Bi. Zahara Abdul Msangi akiwa pamoja na mgeni aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye kwa sasa ni Waziri wa OR-TAMISEMI Mhe.Mohamed Mchengerwa alipotembelea Banda la Maonesho la Halmashauri ya Mkinga katika viwanja vya Mwl. Nyerere Mkoani Morogoro Agosti 04, 2023.





Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Mhe. Kanali Maulid Hassan Surumbu akiwa katika maonesho ya Nanenane kwenye Banda la Halmashauri akipatiwa elimu ya Kilimo cha Bustani ya Mbogamboga pamoja na zao la Korosho Agosti 05, 2023 na Mkuu wa Idara ya Kilimo Ndg. Octavian Moshiro Viwanja vya Mwl.Nyerere Mkoani Morogoro.

## HABARI PICHA: ZIARA YA WAH. MADIWANI MAONESHO YA NANENANE MOROGORO

**KAULI MBIU:**

**"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula."**









Ziara ya Waheshimiwa Madiwani katika maonesho ya Nanenane 08/08/2023, walitembelea Bustani za Halmashauri ya (W) Mkinga na kupatiwa elimu mbalimbali kutoka kwa Maafisa Kilimo na Mifugo wa Halmashauri kuhusu kilimo cha kisasa cha bustani za Mbogamboga, Katani, Mahindi, Ufugaji wa kisasa pamoja na elimu ya Ujasiliamali kutoka kwenye Kikundi cha wanufaika wa mkopo wa 10%.

# MABILIONI YA MHE. RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KUINEEMESHA WILAYA YA MKINGA SEKTA YA ELIMU YA JUU.










**Na: Nassoro Rashid**
**MDC Habari**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya (W) ya Mkinga Mhe. Amani Kasinya Juni 28, 2023 amezungumza na mratibu wa masuala ya jamii kutoka chuo cha Mzumbe Dkt. Christina Shitima wakiwa katika zoezi la utoaji wa elimu, hamasa pamoja na kusikiliza maoni ya Wananchi juu ya ujenzi wa kampasi ya Mzumbe kata ya Gombero wilayani humo.

Mhe. Kasinya ametumia nafasi hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fursa ya mradi huo wilaya Mkinga kupitia usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ufadhili wa mkopo wa shilingi Bilioni 16,554,598,559.00 kutoka Benki ya Dunia kwa ujenzi wa awamu ya kwanza.

> "*Kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Wizara ya Elimu kupitia ufadhili wa mkopo huu, hakika Wilaya ya Mkinga inaenda kuneemeka pakubwa Elimu ya Juu kwani ujenzi wa Kampasi ya Mzumbe Kata ya Gombero ni dhahiri Wilaya yetu inaenda kufunguka kimaendeleo*". *Alisema Mhe. Kasinya.*

Kadhalika Mwenyekiti huyo amesema ameridhishwa na mwitikio wa Wananchi wa vijiji vya kata ya Gombero na Mnyenzani wakati wa zoezi la kampeni ya utoaji wa elimu, hamasa na usikilizwaji wa maoni iliyokuwa ikiratibiwa na jopo la wataalamu kutoka chuo cha Mzuumbe.

**.......INAENDELEA UK. 27**

.....Inatoka UK. 26











Aidha Mhe. Kasinya amesema kampeni hiyo imeleta mwitikio mkubwa kwa Wananchi na kuwapa ari kubwa ya kuendelea kuifungua wilaya kwa kutangaza vivutio vyake mbalimbali ili kuendelea kukaribisha fursa za uwekezaji kwenye sekta ya utalii, elimu, biashara, teknolojia pamoja na miundombinu.

*"Hakika huu ni mradi mkubwa utakaokuja kutufungulia milango mingi ya uwekezaji na kukuza sekta ya utalii, biashara, miundombinu, elimu pamoja na teknolojia wilayani Mkinga na Mkoa wa Tanga kwa ujumla".* *Alisema Mhe. Amani Kasinya*

Sambamba na hilo Mwenyekiti amesema mradi wa ujenzi huo utakapokamilika utakuwa chachu ya kuleta mabadiliko chanya kwa Wananchi kwani ushirikishwaji wa utoaji maoni yao ni dhana ya kuonesha kuwa mradi huo unaangazia kuwanufaisha zaidi mara baada ya kukamilika kwake.

Kampeni hiyo ya kuhamasisha wananchi iliendelea tena katika kata ya Mnyenzani iliyopo wilaya ya Mkinga ili kuifikia jamii na makundi mbalimbali kuweza kuchukua maoni yao na kuwapa elimu ya namna watakavyonufaika kupitia ujenzi wa mradi huo.

## HABARI PICHA: UKAGUZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU




*Mkurugenzi Mtendaji (W) Bi. Zahara Msangi akitoa maelekezo kwa Mhandisi wa Wilaya na Afisa Elimu Msingi wakati akikagua mradi wa nyumba ya Mwalimu (2x1) Shule ya Msingi Jasini iliyopo kata ya Mayomboni imejengwa kupitia Ruzuku toka Serikali Kuu.*

*Agosti 12, 2023*

*Mkurugenzi Mtendaji (W) Bi. Zahara Msangi akikagua Bati zllizotumika kuezekea Madarasa yanayojengwa katika Shule ya Msingi Maramba JKT, Mradi huo umetekelezwa kupitia Fedha za BOOST.*

*Agosti 23, 2023*





*Mkurugenzi Mtendaji (W) Bi. Zahara Abdul Msangi akikagua Madaftari ya Wanafunzi wa Darasa la Nne katika Shule ya Msingi Bamba Estate iliyopo Kwangena Kata ya Mnyenzani Wilaya ya mkinga.*

*Agosti 23, 2023*

## HABARI PICHA: UKAGUZI WA MIRADI KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO

*Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Mhe. Amani Kasinya akisikiliza maoni mara bada ya ukaguzi wa Mradi wa Zahanati ya Mayomboni iliyopo Kata ya Mayomboni inayojengwa kupitia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.*

***Agosti 02, 2023***





*Mjumbe wa Kamati ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii (Mbunge wa Jimbo la Mkinga) Mhe. Dunstan Kitandula akitoa mapendekezo kwa wajumbe ya namna ya kudhibiti uharibifu wa Barabara ya Stakishari- Mwandusi yenye kiwango cha changarawe kwa magari yanayozidisha uzito wa tani.*

*Agosti 02, 2023*

*Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wakiwa katika eneo la Geti la Mtimbwani wakisikiliza maoni kutoka kwa mmoja wa Wakusanya Ushuru pamoja na Askari wa Jeshi la Polisi ya namna ya kuboresha eneo hilo ili liwe chachu ya kuimarisha makusanyo ya mapato na kuongeza usimamizi yakinifu ili kudhibiti mapato ya Halmashauri.*

*Agosti 02, 2023*



## HABARI PICHA : MAFUNZO YA KUKABILIANA NA WANYAMAPORI HATARI - TEMBO



*Mkufunzi kutoka Ekolojia ya Ruvu Same wa Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) akitoa mafunzo ya vitendo kwa vijana 10 kutoka Kata ya Bwiti ya namna ya kutumia kilipuzi chenye mchanganyiko wa pilipili kufukuza Tembo pale wanapovamia katika makazi au mashamba ya Watu.*

*Wakufunzi kutoka Ekolojia ya Ruvu Same wa Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) wakitoa mafunzo ya vitendo ya namna ya kutumia Honi kwa pamoja katika kufukuza Tembo pale wanapovamia katika makazi ya Watu.*

*Julai 06, 2023*





*Mkufunzi akitoa mafunzo ya vitendo kwa vijana ya namna ya kutumia Honi kwa pamoja katika kufukuza Tembo pale wanapovamia katika makazi au mashamba ya Watu.*

*Julai 06, 2023*

*Mkuu wa wilaya ya Mkinga Mhe. Kanali Maulid Hassan Surumbu akimsikilliza Mkufunzi Afisa Mahusiano Ekolojia ya Ruvu Same kutoka Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) Johnson Bernard wakati wa kufunga mafunzo hayo Kata ya Bwiti Wilaya ya Mkinga.*

*Julai 06, 2023*



# MFUKO WA ABBOTT KUFADHILI BILIONI 8.9 KUKARABATI NA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA SHULE YA SEKONDARI MAPATANO WILAYA YA MKINGA



**Na:Nassoro Rashid**
**MDC Habari**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof.Adolf Mkenda (Mb) ameambatana na mgeni wake Rais wa Mfuko wa ABBOTT Duniani Bi. Melissa Brotz Julai 12, 2023 kuzindua mradi mkubwa wa ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Mapatano iliyopo kata ya Mapatano wilaya ya Mkinga.

Akizungumza mara baada ya uzinduzi huo Mhe.Waziri Mkenda amesema mradi huo unaofadhiliwa na Mfuko wa Abbott utagharimu zaidi ya shilingi Bilioni 8.9 hadi kukamilika kwake na kuifanya shule ya Mapatano kuwa ya mfano Mkoani Tanga.

*“ Mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 12 ambapo utahusisha majengo zaidi ya thelathini (30), ni imani yangu kwamba shule hii inakwenda kuwa ya mfano mkoa wa Tanga kutokana na maboresho yake pamoja na kujengwa kwa miundombinu ya madarasa yote yaliyopo sambamba na kujenga madarasa mapya ya kidato cha tano na sita, maabara za kisasa, mabweni, viwanja vya michezo pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu ”.*
*Alisema Mhe. Waziri Mkenda.*

INAENDELEA UK 32

......INATOKA UK. 31





Naye Rais wa Mfuko wa Abbott Duniani Bi.Melissa amesema wanafahamu kwamba kuboresha miundombinu ya elimu ni sehemu ya kuimarisha maendeleo yake hivyo hawatoacha kuendelea kufadhili miradi ya elimu ili maono ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatimie ya kuhakikisha Wananchi wote wanapata elimu bora pamoja na kuboresha maisha yao kwa kuleta maendeleo nchini.

Sambamba na hayo Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Mhe. Kanali Maulid Hassan Surumbu ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Waziri Kindamba alisema,

*"Uwepo wa wadau mbalimbali wa maendeleo katika Mkoa wa Tanga na Wilaya ya Mkinga ni matunda ya kazi nzuri inayofanywa na **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika kuifungua Tanzania, hivyo hatuna budi kuendelea kumuunga mkono na kumshukuru kwa jitihada hizi ambazo zinaendelea kuinufaisha wilaya hii kupitia uboreshwaji wa miundombinu ya elimu lakini pia na sekta nyingine kwa ustawi mpana wa maendeleo ya Wananchi". Aliongezea Mhe. Kanali Surumbu.*

Shughuli hiyo pia ilihudhuriwa na Wajumbe wa Kamati ya Usalama Wilaya, Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Mbunge wa Jimbo la Mkinga ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa sasa Mhe. Dunstan Kitandula, Mwenyekiti wa Halmashauri, Diwani wa Kata ya Mapatano na Viongozi mbalimbali wa Wilaya, Kata na Kijiji.



## FURSA ZA UWEKEZAJI KUPITIA KILIMO

### MAZAO YA VIUNGO



Wilaya ya Mkinga inazalisha mazao ya viungo aina ya Karafuu, Pilipili Manga, Iliki na Mdalasini kwa takribani Tani 349.59 kwa Mwaka katika Maeneo ya Kata ya Kigongoi Mashariki na Kigongoi Magharibi.

### MAZAO YA MAHINDI NA MIHOGO



Wilaya ya Mkinga inazalisha zao la Mahindi na Mihogo kwa wingi katika maeneo ya Kata ya Maramba, Daluni, Gombero, Mhinduro, Bwiti, Mapatano n.k ambapo fursa ya uwekezaji wa Viwanda vya uchakataji wa mazao hayo unahitajika.

### MAZAO YA MKONGE NA KOROSHO



Ardhi ya Mkinga ina rutuba ya kutosha kwa uzalishaji wa wa zao la Mkonge na Korosho kwa wingi hivyo fursa ya uwekezaji wa mazao haya na viwanda vya uchakataji ni kubwa

## FURSA ZA UWEKEZAJI

### FURSA KUPITIA BAHARI



Fursa ya upatikanaji wa Tani 225 wa zao la Mwani kwa mwaka, Samaki takribani Tani 400 kwa mwaka inafungua uwekezaji wa viwanda vya uchakataji wa minofu ya samaki pia uwepo wa hekta 670 ya Misitu ya Mikoko inafungua fursa ya uwekezaji wa biashara ya hewa ya ukaa.

### FURSA YA MADINI YA CHUMVI NA YA UREMBO (TANGA STONE)



Uwepo wa mwambao wa ukanda wa Bahari wenye urefu wa KM 70 unafungua fursa ya uzalishaji wa Madini ya Chumvi na kuna mashamba 38 ya chumvi LAKINI pia hii ndio Wilaya pekee kwa Tanzania nzima kutoa madini ya urembo aina ya Tanga Stone ambayo.

### MNADA WA MPAKANI WA MIFUGO - HOROHORO



Mnada wa Horohoro uliopo Horohoro Kijijini umefungua fursa kwa Wafanyabiashara na Wafugaji kuuza na kununua mifugo aina ya Ng'ombe, Mbuzi pamoja na Kondoo kwa wingi

# FURSA YA UTALII

## HIFADHI YA TAIFA MKOMAZI



Wilaya ya Mkinga inapakana na Hifadhi ya Taifa Mkomazi katika Kata ya Mwakijembe hivyo kuna fursa ya uwekezaji wa Hoteli za Kitalii na Kambi za Kitalii kwa ajili ya kuvutia Watalii wa Nje na Ndani ya Nchi.

## UTALII WA BAHARI



Uwepo wa Matumbawe na Nyasi Bahari katika ukanda wa Bahari ya Hindi eneo la Mkinga (Mwamba Wamba, Mwezi, Chundo, Kiroba) ni kivutio kikubwa cha Utalii wa kuzamia (Diving)



**MPIGA PICHA**
NASSORO RASHID ISSA
KAIMU MKUU KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

**MSANIFU WA JARIDA**
NASSORO RASHID ISSA
KAIMU MKUU KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

**JARIDA HILI HUTOLEWA**

KILA ROBO MWAKA
TOLEO LA ROBO YA KWANZA 2023
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA




# RASIMISHA BIASHARA YAKO PATA LESENI YA HALMASHAURI KUPITIA MFUMO WA TAUSI




JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA



**LIPIA SASA MAPATO YA HALMASHAURI YAKO** 👍